# *Kuweka Mhudumu*

Yeye ni Mungu, basi. Yupo kila mahali. Unaona? Yuko kila mahali. Nilifikiri tu ningeliacha tu lining'inie nione jinsi lilivyoshikilia, mwajua. Yeye yupo kila mahali. Yeye... Hilo linamfanya Yeye kuwa Mungu, maana Mungu pekee ndiye anayeweza kuwa kila mahali. Kwa hiyo Yeye alisema, "Mwana wa Adamu ambaye sasa yuko Mbinguni." Unaona? "Hakuna mtu aliyepaa juu, ila Yeye aliyeshuka kutoka Mbinguni, yaani Mwana wa Adamu ambaye yuko Mbinguni." Huyo hapo, amesimama juu ya nyumba, lakini yuko Mbinguni. Unaona? Yeye yupo kila mahali, hilo linamfanya kuwa Mungu. Hicho ndicho kitu tu kinachoweza kuwa kila mahali, ni Mungu.

2 Sasa, usiku wa leo, nilipata tu sehemu ya mwisho kabisa ya ujumbe mzuri sana wa Ndugu Neville kwa kanisa. Mungu na aubariki na auongezee. Na, unaona, aliwaacha mkibakia pale, kwenye kutafakari. Hilo ni jema. Wekeni hilo moyoni mwenu, daima.

3 Na sasa, tutakuwa na ushirika usiku wa leo. Na huo ndio wakati ambao sisi sote tunaufurahia, nina hakika. Nafikiri ndio furaha ya moyo wa Mkristo, ni kujua ya kwamba anakuja kutimiza amri ambayo Yesu alituachia. Kuna maagizo mawili ambayo Yesu alituachia, mambo mawili. Moja ya hayo ni ibada ya ushirika, na hilo lingine ni ubatizo wa maji. Vinginevyo, hakuna "gusa, shika," hakuna lingine lililoachwa kwake, unaona, hakuna vitubio na kujikokota kwa magoti yako, na mambo haya mengine yote. Ni—ni ubatizo tu wa maji na ushirika. Kwa hiyo daima tuna furaha sana kufikia jambo hili.

4 Ninaamini Biblia ilisema, "Heri yule anayetimiza amri Zake, wao wana haki ya kuingia kwenye huo Mti wa Uzima, kwa kuwa katika Mji huo, Mji Mtakatifu; kwa kuwa huko nje wako mbwa, waasherati, na kadhalika, ambao watatupwa nje."

5 Halafu ibada ya ushirika daima ni jambo zito sana, kwa maana linatufikisha kwenye shindano la kuamua, unaona, kama tutakavyosoma hivi punde, katika Maandiko.

6 Tunaye Ndugu Brown anayeketi hapa, usiku wa leo, Ndugu Dauch, na Ndugu Brown, na Ndugu McKinney. Siwezi kukumbuka majina ya hao ndugu wengine wanaoketi kule. Lakini tuna furaha kuwa pamoja nao kutoka huko Ohio. Ninamwona Ndugu Pat Tyler hapa, na Ndugu Stricker kule nyuma, wahudumu wa Injili, walio nyuma yangu. Ndugu Collins, pia, na Ndugu Hickerson.

7 Sasa, Ndugu Stricker, vipi kidole cha mkeo? Kinapata nafuu. A-ha. Alipata ajali, naye akanipigia simu juzi usiku. Na wakati nilipoingia, kutoka kwenye simu nyingine, ilikuwa ni kama

saa sita, saa saba, wala sikumpigia simu wakati huo; asubuhi yake. Alikuwa anashona na kwa njia moja ama nyingine, akajichoma mikononi kwa sindano, ikaingia kwenye mfupa ama kitu kama hicho. Ndipo akajaribu kuivuta namna *hii*, kutoka kwenye cherahani, cherahani ya umeme. Na, alipojaribu kuivuta, ikavunjika namna *hii*. Ndipo akajaribu kuing'oa kwa meno yake, maskini mama huyo, akijaribu kuing'oa, kwake, akaivunja mahali pengine, mkononi mwake.

8 Basi akasema, "Omba tu na itakuwa sawa." Ninapenda hiyo imani halisi, kushikilia pale mahali hapo. Ninaipenda hiyo. Dada Stricker ni maskini Mkristo mpendwa, nami simwoni hapa usiku wa leo, kwa hiyo ninaweza tu kuzungumza juu yake. Yuko? Loo, vema, afadhali ninyamaze. Yuko hapa, pia. Sawa. Vema, tunafikiri ndivyo ulivyo, hata hivyo, Dada Stricker.

9 Sasa, Ndugu McKinney aliomba, ninaamini, hapa muda fulani uliopita, ya kwamba. . .Tunasikitika. Billy Paul ndiyo kwanza anikumbushe juu ya jambo hilo, juu ya kule kuweka muhudumu kwenye huduma, ama kwa maneno mengine, kuweka muhuduma Kimaandiko kutoka maskanini. Hiyo ni kweli, Ndugu McKinney? Nilifahamu jambo hilo vizuri? Sasa, cheti chake hutolewa.

10 Sasa, asubuhi ya leo, sikujua nitakuwa hapa kuzungumza. Lakini baada ya kuja hapa, na ndugu yetu hapa, aliyejaa neema na upendo, aliniomba nije na nizungumze. Nasi tukaeleza kwamba kanisa lilikuwa ni kitu gani, na kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa ni nini, na ni nani aliye Nao, na ni nani asiyekuwa Nao, na jinsi unavyojua unapokuwa unao Huo. Unaona? Kwa hiyo, kama hukupata Ujumbe huo, basi hao vijana, wao wanazo hizo kanda pale, ambazo zinaweza kwenda kwenye kanisa letu, maana ni ya Mafundisho matupu, toka mwanzo hata mwisho.

11 Na ndipo nikatoa tamshi hili, ya kwamba, hakuna kitu kama madhehebu ya Kanisa. Hakuna kitu kama hicho. Ni loji la madhehebu. Wewe unazaliwa tu katika Kanisa. Na wakati mtu fulani anaposema, "Mimi ni Mpresbiteri," wewe ni wa loji la Kipresbiteri. Unaona? Kwa sababu unazaliwa. . . "Mimi ni Mbatisti." Wewe ni wa loji la Kibatisti, si Kanisa la Kibatisti. Hakuna kitu kama hicho. Nasi tuliligeuza hilo moja kwa moja, na tukaona katika Biblia, ya kwamba hata kusema kitu kama hicho ni kukufuru. Hiyo ni kweli. Hebu lisome moja kwa moja kutoka kwenye maandiko asili ya mkono kutoka katika Emphatic Diaglott, ya kwamba Biblia ilisema ya kwamba ninii. . .ya kwamba nguvu hii, inayoitwa kanisa, "imejaa majina ya makufuru." Unaona? Wakijiita wenyewe ni Wakristo na kujifanya ni Wakristo, na kuishi tu maisha ya namna yo yote. Mnaona? Na bila shaka inalingana na ndoto ambayo dada fulani hapa kanisani aliota, tuliyoelezea hapa asubuhi ya leo. Sasa, nyakati za Biblia, jinsi walivyoweka wahudumu,

ilikuwa ni kwa kutambua karama ya Mungu katika mhudumu huyu, huduma.

12 Hapo ndipo ninapofikiri ya kwamba Watakatifu wetu wa Siku Hizi Baadaye. . .Ama si Mtakatifu wa Siku za Hizi. Samahani. Ndugu wa mvua ya vuli, walifanya kosa baya sana kwa kuwekea mikono na kusema, "Tunakupa karama ya uponyaji. Tunakupa karama ya unabii." Hakuna kitu kama hicho.

13 "Karama na miito havina majuto." Mungu hutoa. "Mungu ameweka Kanisani mitume, manabii," na kadhalika. Unaona? Hakuna kitu kama mtu mmoja kumpa mwingine karama. Karama zinatoka kwa Mungu, Mungu peke yake.

14 Na kuja Kanisani, unazaliwa ndani Yake. Hakuna njia nyingine ya kuingia ndani Yake. Na ndipo wewe ni mmoja wa familia, na wa Mungu, ukiwa mwana na binti wa Mungu. Si madhehebu, bali m—mmoja wa familia.

15 Sasa, katika nyakati za Biblia, kama anavyosema, wanachukua Maandiko pale wakati Paulo alipomwambia Timotheo ya kwamba alipewa karama.

16 "Vema," alisema, "ilitoka kwa bibi yake Loisi. Unaona? Alipokezwa karama iliyotoka kwa bibi yake Loisi."

17 Waliona ndani yake, yeye akiwa ni Mkristo hodari, pia, karama ya kunena. Nao wakamwekea mikono, kwa kuitambua. Wazee wa kanisa walimwekea mikono, wakimtambua mtu huyu; na kumweka mahali pake, huduma ya kimitume, ya kumwekea mikono, apate kwenda kuhubiri Injili. Akatumwa, kwa ushahidi wa hawa ndugu, kwamba wao waliamini ya kwamba karama ya Mungu ilikuwa ikitenda kazi ndani yake. Hivyo ndivyo walivyofanya pia kwa wale wahudumu, kwa kuwekea mikono, na kumpa mkono wa kuume wa ushirika; kwamba, watafanya kazi pamoja, kama mapatano mbele za Mungu, ya kwamba waliona karama ikitenda kazi katika ndugu huyu, ya kwamba aliitwa kwa ajili ya jambo fulani. "Nasi tunaamini jambo hilo." Nao wakamwekea mikono, kwamba Mungu ambariki. Na ilikuwa ni kibali.

18 Ni kama tu vile nisingeninii. . .Mtu fulani daima amenishtaki, kuwa mimi ni "Yesu Pekee." Yesu pekee, katika ubatizo, kwa kutumia Jina la "Yesu Kristo," bila shaka ninakubaliana na jambo hilo. Lakini wakati unapobatizwa "ili uzaliwe mara ya pili," siwezi kuamini jambo hilo, ya kwamba maji husamehe dhambi. La. Ninaamini Damu ya Yesu Kristo hulipia dhambi. Kwa hiyo, si ubatizo wa kuzaliwa mara ya pili, lakini ni ubatizo wa ungamo. Ubatizo wako ni ungamo lako, ya kwamba unaamini, ya kwamba kazi hii ya ndani ya neema imekwisha kutendeka.

19 Kwa hiyo, ninaambatana na Wabatisti wanaposema, wakiingia katika kanisa la Kibatisti, unafanya maungamo yako,

ukabatizwa katika ninii. . .katika kanisa lao. Hilo lingekuwa ni sawa, mradi tu umebatizwa katika kanisa hilo, hiyo imani ya Kibatisti.

Lakini, sasa, kuingia katika Kristo, unabatizwa kwa Roho Mtakatifu, kuzaliwa mara ya pili.

20 Ndipo unapokuja kanisani, jambo pekee ambalo ubatizo unafanya, ni ninii tu. . .ni ushuhuda ya kwamba unaamini ya kwamba—ya kwamba Kristo alikufa na akafufuka tena, siku ya tatu. Nawe umemkubali kama Mwokozi wako binafsi, na umekufa tena kwa mambo ya ulimwengu. Ukiuonyesha ulimwengu ya kwamba ulikufa pamoja Naye, na umefufufka pamoja Naye katika ufufuo. Ni tendo la nje ya kwamba kazi ya ndani ya neema imefanywa. Haina uhusiano wo wote na kukupa wewe wokovu, maana Damu ya Yesu Kristo. . .Jambo pekee lililokupasa kufanya, ni, kusema tu, nenda ukabatizwe, na haingembidi Yesu kufa. Ilichukua mauti kuleta Uzima, daima.

21 Kwa sababu, tunaishi tu kwa mauti. Kitu cho chote kinaweza kuishi tu kwa mauti. Tunaishi kwa vitu vilivyokufa, tunapovila. Kila siku unapokula, kitu fulani hakina budi kufa kusudi upate kuishi, kimwili. "Vema," unasema, "mimi sili nyama." Vema, sijali unakula nini, wewe. . .kitu fulani kilikufa. Hiyo ni kweli. Ukila kiazi, kilikufa. Ukila sukumawiki, zilikufa. Ukila mkate, ngano ilikufa, mahindi yalikufa, cho chote kile. Namna fulani ya uhai hufa, kwa maana unaishi tu kwa kitu kilichokufa.

22 Halafu basi kama huna budi kuishi, kwa kawaida, kwa kitu kilichokufa, ni zaidi sana jinsi gani ilihitaji kitu kilichokufa, upate kuishi Milele? Kristo alikufa, kusudi mwanadamu apate kuishi tena. Na hilo pekee ndilo lenye Uzima, kuwa katika Kristo.

23 Sasa, haya matendo ya nje. Nasi tunamwona Ndugu McKinney, ambaye ni mhudumu wa Kimethodisti aliyewekewa mikono, ambaye ameona Nuru ya Injili yote. Tunamwamini, ndugu mzuri sana, mwenye familia nzuri. Naye amekuja kwetu. Naye anajaribu kushikamanisha kundi moja dogo pamoja, huko—huko Ohio, pamoja na Ndugu na Dada Dauch, na hao ndugu wengine huko. Nasi tunafurahia kuwa naye hapa. Nasi tunaamini kwamba yeye ni mtu aliyeitwa na Mungu. Kwa hiyo, kama tulivyowafanyia Ndugu Jim Sink, Ndugu Graham Snelling, Ndugu Junior Jackson, Ndugu Willard Crase, kwa kila mtu tuliyemtuma kutoka hapa, tunawaleta mbele ya kusanyiko hili, tukitoa ushuhuda huu, kama vile mlivyosikia. Tunawawekea mikono, kwamba tunaamini ya kwamba wameitwa na Mungu, na kulipa jambo hilo kibali chetu, na kuomba baraka za Mungu ziambatane nao.

24 Ukiona kitu tofauti ndani, nje ya Biblia; kama ukikipata, kitakuwa nje ya Biblia. Hivyo ndivyo walivyofanya jambo hilo hasa katika wakati wa Biblia, ilikuwa ni kuwawekea

mikono, katika kuwaweka. Waliwawekea mikono mashemasi na kuwaweka kanisani. Kila kitu kilikuwa ni kwa kuwekea mikono, si kutia sahihi lundo fulani la makaratasi na kujiunga na kanuni fulani ya imani, ama kitu kama hicho. Walimwekea mikono, na kumwachilia katika Roho Mtakatifu, wakamwacha aende. Amina. Mungu akamwongoza jinsi anavyotaka. Hivyo tu. Hilo, hivyo ndivyo tunavyoamini katika kufanya jambo hilo.

25 Ndugu McKinney, tuna furaha, usiku wa leo, kukuona ukija jinsi ulivyokuja. Na jambo unalojaribu kufanya, kutimiza jambo fulani kwa ajili ya Kristo.

26 Wala hatutengi kanisa lo lote, mfuasi ye yote wa kanisa lo lote, la Kimethodisti, Kibatisti, Kipresbiteri, Kikatoliki, ye yote yule. Tunaamini ya kwamba Roho wa Mungu humshughulikia mtu binafsi. Na katika kila kanisa kuna Wakristo, kote kote katika ulimwengu mzima wa kanisa, kama unavyoitwa, leo. Ninaamini kuna Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteri, Waluteri, wanaompenda Mungu. Na jambo pekee wanalojua juu Yake, wanaishi karibu sana wawezavyo, karibu sana wajuavyo kuishi, ama walivyofundishwa kuishi. Watu wengine wanafikiri yote wanayopaswa kufanya ni kuandika tu jina lao katika kitabu, na kujiunga na kanisa, hivyo tu ndivyo inavyowapasa kufanya. Mama yangu alikuwa mfuasi wa kanisa fulani. Baba yangu alikuwa mfuasi wa kanisa fulani. Vema, hilo, unaona, hilo tu ndilo wanalojua kufanya.

27 Lakini Yesu alimwambia huyu kiongozi wa Wayahudi, asubuhi ya leo, "Mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi hata kuuona Ufalme wa Mungu," haidhuru wewe ni mfuasi wa kanisa lipi. Naye alisema, akazungumza juu ya Kuzaliwa upya.

28 Alisema, "Ati mimi, mzee, kuingia katika tumbo la mama yangu, na kadhalika, nizaliwe tena?"

Akasema, "Wewe ni mwalimu katika Israeli, wala hujui mambo haya?"

29 Angalia jinsi kanisa la ulimwengu linavyounda madhehebu na kupotoka, mpaka linakuwa ni kundi tu la kanuni za imani? Hizo ni nadharia zilizobuniwa na wanadamu zikaingizwa katika mambo ya kiroho. Na mambo ya kiroho yatajitenga nazo yenyewe, kila wakati. Wewe, kama msemo wa kale usemavyo, huwezi kuchanganya mafuta na maji. Hayatachangamana kamwe, hivyo tu. Hakuna, hakuna vitu pale vitakavyochanganyikana.

30 Na hivyo ndivyo iliyo sasa. Tunaamini ya kwamba Roho Mtakatifu huwaita watu. Roho Mtakatifu huwateua watu. Haidhuru, tungeweza kuweka mikono juu ya Ndugu McKinney, ama mhudumu mwingine ye yote yule, saa baada ya saa, siku nzima, na kumpa makaratasi marefu ambayo angeweza kutia sahihi nadhiri za kanuni za imani, hilo halitamfanyia kitu cho chote. Lakini, hebu Roho Mtakatifu na amguse, mara moja.

Imekwisha. Hilo latosha. Hakuna mtu anayepaswa kumwambia jambo jingine lo lote. Huyoo ametoweka. Unaona? Imekwisha. Halafu basi, jambo pekee tunaloweza kufanya, ni kufanya ushirika, ya kwamba tunatambua ndugu yetu yuko katika nafasi hiyo.

31 Mungu na akubariki, Ndugu McKinney. Utakuja hapa, mbele, kwa muda kidogo tu.

32 Ndugu Neville, Ndugu Collins, wahudumu, kama mngetaka kusimama hapa karibu, tungefurahi mkija hapa, kwa dakika moja.

33 Kama mtakuja tafadhali na mwelekee kwenye kusanyiko, Ndugu McKinney, moja kwa moja namna *hii* hapa.

34 Ni wangapi wanaomjua Ndugu McKinney, wamekutana naye hapa? Ni wangapi wanaamini kwamba ni mcha Mungu? Inua mkono wako. Bila shaka.

35 Tuna furaha, usiku huu, Ndugu McKinney, tunaposimama kando yako hapa, karibu nawe, pamoja na kusanyiko hili, kujua ya kwamba umekubali u—ushirika wa mahubiri ya Injili yote; ya kwamba umeamua, kwa neema ya Mungu, kushikilia bendera ya Biblia. Haidhuru cho chote kitasema nini kuihusu Hiyo, utadumisha msimamo wako juu ya Neno la Milele la Mungu. Halafu haidhuru ni madhehebu gani yanayojaribu kuliweka kando, wewe utasimama vile vile jinsi lilivyoandikwa. Utadumu sawasawa Nalo. Hiyo ndiyo. Hivyo ndivyo tunavyoamini hapa. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Wote wanaliamini namna hiyo. Neema ya Mungu na iwe pamoja nanyi daima.

36 Sasa, omba ombi lako mwenyewe, hivi kwamba Mungu atamkubali ndugu yetu.

37 Kwa kuwa, Nuru za jioni zinaangaza, na jua linashuka upesi. Kuja kwa Kristo kumekaribia. Maombi yangu manyenyekevu ni kwamba Mungu ataiamsha nafsi ya mvulana huyu kwa ubatizo wa Roho, na amtie mafuta, atoke aende huko nje na kuokoa makumi elfu ya nafsi, kabla ya kule Kuja kwa Bwana. Mungu anajua tunamhitaji katika huduma.

38 Tunakutaka ujue, Ndugu McKinney, kama kanisa hili na kundi hili la watu hapa. Kanisa ni kundi la watu waliokusanyika pamoja, bila madhehebu. Hilo halimfanyi mtu hata mmoja hapa, haiwezekani kwa sababu ati unakuja hapa, ama kanisa lo lote lile, lingekufanya mfuasi wake. Kuna njia moja tu ya kuwa mshiriki wa Mwili wa Kristo, hiyo ni, unazaliwa ndani Yake, kwa Roho Mtakatifu. Na tunaamini ndugu yetu amezaliwa katika Mwili huu, ana wito maishani mwake kuhubiri Injili. Sisi ni mashahidi wa jambo hili, usiku wa leo, ya kwamba tuko nyuma yako, pamoja na maombi yetu. Mungu akuongoze, ndugu yangu.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

39 Baba yetu wa Mbinguni, linatia nguvu tu nafsi yangu ninapomwona m—mhudumu akija, akitambua Injili yote. Kwamba Kristo alisema, ya kwamba mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Lake halitashindwa. Ndipo tunaona, Wewe ulisema pia, ulipomaliza kuandika kile Kitabu, "Yeye atakayeongeza neno moja kwenye Kitabu hiki, ama kutoa cho chote Kwake, huyo ataondolewa (sehemu yake) kwenye Kitabu cha Uzima."

40 Ndugu yetu McKinney ameona jambo Hili. Na katika kundi la ndugu, wa mahali alipokuwa akiabudia, alileta Kweli aliyoona katika Maandiko. Hakuna mtu angaliweza kustahimili jambo Hilo, lakini hata hivyo madhehebu hayangeweza kuvumilia jambo Hilo. Kwa hiyo anachagua mwenyewe, aidha kufuata yale mwanadamu amesema, ama kile Mungu amesema. Mungu, na—nakushukuru kwa kumpa ujasiri wa kuchukua yale Mungu alisema. Kwa maana Biblia ilisema, "Na neno la kila mwanadamu na liwe uongo, na la Mungu liwe Kweli." Naye ameamua kushikilia jambo Hilo.

41 Na ili kuonyesha ushirika wetu pamoja naye, ama kusimama pamoja naye katika majaribu yake, kufurahi pamoja naye katika ushindi wake, tuko hapa kama askari pamoja. Mimi, pamoja na mchungaji wa maskani hii, tunamwekea mikono, katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba utambariki ndugu yetu. Mfanye hai katika Roho. Mjaze na nguvu, kuhubiri Injili. Mpe ishara na maajabu zitakazofuata huduma yake. Na jalia awe chombo katika mkono Wako, kilichowekwa wakfu Kwako, katika siku hizi za mwisho, kuokoa maelfu ya watu waliopotea wanaotangatanga gizani leo. Tujalie, Bwana. Hili ndilo ombi letu, na imani yetu katika ndugu yetu, na matumaini yetu na imani yetu Kwako, ya kwamba utajibu maombi yetu, kwa ajili ya saa hii kuu yenye mahitaji katika huduma ya ndugu yetu. Katika Jina la Yesu tunamtuma. Amina.

42 Mungu akubariki, Ndugu McKinney. Na neema ya Mungu na ikae nawe daima, na ikupe shauku ya kweli ya moyo. Mungu awe pamoja nanyi.

43 Huko ndiko kuwekwa kwenye huduma ninakojua, kwa Biblia, mkono wa kulia wa ushirika. Wote wanaompa Ndugu McKinney mkono wa kulia wa ushirika, katika kanisa hili, inua mkono wako. Maombi yetu, usaidizi wetu, ni kukusaidia kusimama juu ya jambo ambalo ni Neno la Milele la Mungu.

44 Ambalo, "Mbingu zote na nchi zitapita, bali lingali litakuwa limesimama." Kwa sababu, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu."

45 Neno lilisema, "Mimi ni Mzabibu, ninyi ni matawi." Na Uhai ule ule uliokuwa katika tawi, katika Mzabibu, unapigapiga katika Mzabibu na kutoa Uhai ule ule, pamoja na matunda yale yale, pamoja na kazi zile zile, pamoja na jambo lile lile.

Ninajua ni Kweli, kwa sababu nimeona likitimia. Amina na amina. Ninapenda ile njia nzuri ya kale ya Injili. Naam, bwana.

46 Sasa huenda imekawia kidogo, inaelekea saa tatu na nusu, lakini sasa tutafanya ibada ya ushirika.

47 Sasa, tunauita "ushirika," lakini si ushirika. Ushirika ni kuongea, kuzungumza. *Kuzungumza* ni wakati tunaponyamaza na kuongea na Bwana, kuongea. Lakini, sasa, hii inaitwa "meza ya Bwana." Sijui jinsi baadhi ya hawa watu wa kisasa, ambao hawasemi "chakula cha jioni" tena, na wanakiita "chakula cha mchana," jinsi watakavyofanya sasa? Unaona? A-ha. Unaona? Naam, bwana. Ni meza ya Bwana. Tunaamini tu Biblia jinsi inavyosema jambo Hilo.

48 Nasi tunawatakeni mjue, ya kwamba Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteri, Mluteri, cho chote ulicho, unaalikwa, na ndugu pamoja nasi, kama umezaliwa na Roho wa Mungu, kusimama hapa, kufanya ushirika pamoja nasi.

49 Tunaamini ya kwamba huu unawakilisha mwili wa Yesu Kristo uliovunjwa. Na tunaamini ya kwamba Mkristo ana wajibu wa kuula. Tunaamini ya kwamba mtu asiyeishi maisha mema, anayekuja na kuula, pasipo kuishi vizuri, anakula na kunywa hukumu yake binafsi, kwa kutoupambanua Mwili wa Bwana. Hiyo ndiyo sababu makanisa hayo yanayojiita Wakristo, yalikutwa, katika Biblia, "Yamejaa majina ya makufuru." Mnaona? Kwa sababu, kula ushirika, na kutoka kwenda na kuishi maisha yo yote, inaleta jiwe kubwa zaidi la kujikwaa kuliko baa zote zilizoko nchini kote.

50 Unaona malaya barabarani, unajua yeye ni nani. Unaangalia jinsi anavyotenda na anavyovalia, unamjua. Lakini Mkristo hapaswi kufanya jambo hilo—jambo hilo. Kama ukiona ma—ma—ma—mahali hapa chini, panaposema, "Ghala la kupakia! Divai, wiski," na kadhalika. Unajua hiyo ni nini. Hapo ndipo—hapo ndipo mahali hapo. Hilo ni sawa. Kucheza dansi, mpira, kadhalika, unajua hicho ni nini. Lakini unawatarajia watu mle ndani kuwa wanakunywa, wanacheza kamari, wanadanganya, wanaiba, cho chote kile. Hicho ni—ni kiota cha pepo wachafu.

51 Lakini unapoona mahali panapokiri kuwa wana na binti za Mungu. Unaingia mle, na jambo la kwanza, unawaona wakikana Maandiko yenyewe kabisa, kuafikiana na. . .kwa kuwa hayaafikiani na kanuni zao za imani. Unawaona wakija kule ndani, na kuzungumza juu ya kazi ya Mungu kufanya jambo fulani, na kuicheka. Huyo hapo yule mnafiki. Naam. Hicho hapo ndicho kile kitu kiovu. Na kuwaona hao watu wakija na kufanya ushirika, na kwenda moja kwa moja huko mitaani na kuishi kama tu wengine wao, hilo ndilo jiwe lililo kuu sana la kujikwaa, hilo hapo.

52 Nilihubiri hapa, si muda mrefu uliopita, "Kuadhirika Hukumuni." Huyo muuza pombe haramu hataadhirika

atakaposikia hukumu yake ya kwenda jehanamu. Hataadhirika, wala mdanganyifu wala mwizi. Lakini mwenye kuadhirika atakauwa ni yule aliyedhania alikuwa mwenye haki. Huyo ndiye atakayeadhirika. Bila shaka kutakuwa na wengi wa hao. Tunajua jambo hilo.

53 Na Mungu na azirehemu nafsi zetu. Hili ni jambo lisiloweza kuchezewa. Majuma machache yaliyopita, kulikuwako na mmoja hapa aliyeketi kati yetu, akiwa mzima, ndugu mzuri, Ndugu Taylor. Yuko Utukufuni, usiku wa leo, aliondoka katika muda wa dakika moja. Na sasa tunajua ya kwamba siku moja tutaondoka, kwa hiyo sasa huu ni wakati wa kuishi maisha mema. Huu ndio wakati.

54 Basi mnakumbuka somo la asubuhi ya leo? Sifa hizi hazina budi kuwemo kabla hata lile Jiwe la Kufunika halijaja juu yake. Loo, waweza upige makelele. Waweza uimbe. Waweza unene kwa lugha, na ucheze dansi. Hilo halina uhusiano wo wote na jambo hilo. Mpaka mambo haya, yamethibitishwa Kimaandiko na kutiwa muhuri ndani yako, Roho Mtakatifu anakutia muhuri kama mtu binafsi, ndipo wewe ni mwana na binti.

55 Tumewasikia watu wakinena kwa lugha, ambao hawakuwa na Roho Mtakatifu. Mnajua jambo hilo.

56 Nimewasikia wachawi wakinena kwa lugha. Waganga wa kienyeji wakinena kwa lugha, na kunywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kumwita Ibilisi. Naam, bwana. Kwa hiyo, wewe, hilo si . . . Nimeona wachawi, walozi, nikaona wakati penseli ilipowekwa chini, na ikakimbia huku na huku kwenye bomba la moshi na kucheza ule "nyoa na kukata nywele," na kuandika katika lugha zisizojulikana. Na jamaa fulani amesimama pale, wakati ikiandika tu huku na huku, na kuandika, na kusema yale hasa iliyokuwa ikisema. Sasa, unajua huyo si Mungu. Nawe unajua mambo hayo yote.

57 Kwa hiyo kunena kwa lugha hakumaanishi wewe ni—wewe, ni wa Mungu. Kufanya miujiza hakuthibitishi wewe ni wa Mungu.

58 Ni lile jambo, matunda ya Roho, yanayothibitisha ya kwamba wewe u ndani ya Mungu, unapoona hayo Maisha yametiwa Muhuri na Roho Mtakatifu.

Mungu, tujalie. Hebu hao wawe ni sisi. Kama tumetenda dhambi, Baba mkuu wa Mbinguni na atusamehe.

59 Nitasoma baadhi ya Maandiko, yale Yesu aliyosema nasi kwa Roho. Sasa, nitayasoma kutoka mlango wa 11 wa Wakorintho wa Kwanza. Na nitaanza kwenye kifungu cha 23. "Kwa maana nalipokea kwa Bwana . . . " Ninazungumza sasa kama Paulo anavyozungumza.

*. . . mimi nimepokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, Ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate,*

*Naye* aliposhukuru, *akaumega, akasema, Twaeni, mle: huu ndio mwili wangu, uliovunjwa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*

*Na vivi hivi pia baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.*

*Maana kila mwulapo mkate huu, na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.*

*Basi kila aulaye mkate huo, na kukinywea kikombe hicho cha Bwana, isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.*

*Kwa* hivyo *mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe.*

*Maana alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili wa Bwana.*

*Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, . . .watu kadha wa kadha wamelala.*

*Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa.*

*Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia.*

*Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo mpate kula, mngojane;*

*Mtu akiwa na njaa, na ale nyumbani kwake; msipate kukutanika kwa hukumu. Na hayo yaliyosalia nijapo nitayatengeneza.*

60 Ningetaka kusema hivi juu ya ushirika. Sasa, huo ndio kikwazo kikuu, kati, sababu ambayo leo kanisa Katoliki na kanisa la Kiprotestanti hayawezi kuungana, ni kuhusu jambo lili hili. Mkatoliki huuchukua kama misa. Naye anatumainia, kwa matendo fulani mema, ya kisheria ambayo ametenda, na kwa kutimiza agizo hili, ya kwamba atasamehewa dhambi zake. Mprotestanti anauchukua, kwa shukrani, ya kwamba dhambi zake zimesamehewa, kwa kuwa ametii amri.

61 Sasa, ule mkate, Mkatoliki husema ya kwamba ni mwili kabisa. Na hili ndilo Andiko wanalotumia, kutoka katika Wakorintho hapa, Wakarintho wa Kwanza 11.

Kasema, "Yesu alisema, 'Twaeni mle: huu ni mwili Wangu.'"

Mprotestanti anasema, "Unawakilisha ule mwili."

62 Mkatoliki anasema, "Ni mwili. Na, kwamba, ka—kasisi amepewa uweza wa Mungu wa kugeuza ule mkate mwembamba kuwa mwili halisi wa Kristo."

63 Sasa, kama ukiangalia, mwili wa Yesu haukuwa umetolewa, wakati aliposema, “Huu ni mwili Wangu.” Yeye alivunja mkate na kusema, “Twaeni mle: huu ni mwili Wangu.” Mwili wake ulikuwa bado haujavunjwa. Kwa hiyo, Maandiko ya—yao wenyewe, kitu chao wenyewe wanachotumia, kinapasisha hukumu juu ya fundisho lao. Unaona? Yesu alichukua mkate akaumega, na kuwapa wao, kasema, “Huu ni mwili Wangu. Twaeni mle.” Naye huyu hapa amesimama hapa, katika mwili Wake. Haukuwa kamwe umevunjwa bado. Aha! Hata hivyo, Maandiko hayatasema uongo. Yatajiweka dhahiri daima. Kwa hiyo, tunaamini jambo hilo.

64 Nasi tunaamini ya kwamba tunapokutanika, Yeye alisema, “Ngojeaneni.” Kwa neno lingine, “Ngojeaneni ninyi kwa ninyi.” Neno *ngojea* linamaanisha “kusubiri.” “Ngojeaneni ninyi kwa ninyi.”

65 Sasa, kama ilivyokuwa desturi yetu, tunalichukua Andiko hilo hivi. Ya kwamba, tunapofanya jambo hili, ya kwamba tunainamisha vichwa vyetu tu, na kusanyiko linatuombea sisi wachungaji. Sisi wachungaji tunaliombea kusanyiko letu. Hivyo ndivyo tunavyongojeana, kwa kuhudumiana, kwa kuomba.

66 Unaomba, “Mungu, msamehe mchungaji wangu. Kama kuna jambo lo lote maishani mwake ambalo wao—wao wamefanya, wasamehe kwa jambo hilo. Wasamehe. Hawakumaanisha kufanya jambo hilo.”

67 Nasi tunarudi moja kwa moja, wachungaji, tukiliombea kusanyiko letu, “Mungu, hili ndilo kundi dogo ulilotupa kulichunga. Kama kuna jambo lo lote baya maishani mwao, liondoe, Baba. Wao . . . Kwa hiyo sisi sote tunaweza kusimama pamoja hapa pande zote, kushiriki faraghani, tukijua ya kwamba tunakuja hapa, tutimiza agizo la Mungu, na kufanya ushirika.” Ninafikiri ni wakati mzuri sana wa ushirika.

68 Hebu na tuombe sasa tunapoinamisha vichwa vyetu. Tuombeeni, polepole, tunapowaombea. [Ndugu Branham na kusanyiko wanaomba polepole kwa sekunde arobaini—Mh.]

69 Baba, tunapofanya ushirika huu, kama tunavyouita ushirika, ni katika kukukumbuka Wewe. Na wakati mkate huu mdogo mwembamba uliopigwapigwa utakapogusa ndimi zetu na kuingia katika kinywa chetu, jalia tutambue ya kwamba Yeye alichubuliwa na kupondwa, akararuliwa kwa ajili ya dhamb zetu. Na lile pazia lililomficha tusimwone, sasa Yeye yumo ndani yetu, Roho Mtakatifu.

70 Na wakati tunapopokea divai, jalia tutambue ya kwamba ilikuwa kwa kupigwa Kwake kwamba tumeponywa, kwa Damu Yake tunaokolewa, Uzima uliokuwa katika Damu.

71 Sasa, Baba, tukusanye pamoja kwa ajili ya wakati huu wenye uchaji, ukitusamehe dhambi zetu. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

72 Ninaamini sasa ya kwamba wazee, mmoja wao, atakuja hapa mbele. Ya kwamba, ninaamini, ya kwamba kwa kawaida hiyo ilikuwa ni kazi ya Ndugu Taylor, pia, (sivyo?) kuja mbele, kuwaalika kwenye ushirika. Sijui ni nani angepachukua mahali hapo? Ndugu Tony, unaweza kufanya hivyo? Ndugu Zabel, hapa, atakuja mbele na kuongoza, safu kwa safu, tunaposonga mbele, tukifanya ushirika, tunarudi kwenye viti vyetu.

73 Je! unajua ya kwamba ushirika una uponyaji wa Kiungu ndani yake? Wakati Waisraeli, katika mfano, walipofanya ushirika, na kutembea kwa miguu miaka arobaini. Na wakati walipotoka jangwani, hapakuwapo na hata mmoja aliyekuwa mnyonge kati yao, watu milioni mbili na nusu. Kuna nguvu za uponyaji katika ushirika.

Kila mtu anakaribishwa sasa.

74 Na dada yetu, kama atakuja kwenye piano, apige wimbo huu.

> Damu imebubujika,
> Ni ya Imanueli,
> Wakioshwa wenye taka,
> Husafiwa kweli.

75 Dhambi zenu na zisamehewe, enyi watoto. Naomba neema ya Mungu daima iwe pamoja nanyi, tunapokuwa katika safari hii. Naomba sote tukutane kwenye ng'ambo ya pili, tukiwa wenye furaha na vijana tena. Amina.

76 [Mpiga piano anaanza kupiga *Damu Imebubujika*, naye Ndugu Branham na kusanyiko wanatulia kwa dakika moja wakati watu wa kwanza wanakuja mbele kupokea mkate wa ushirika na divai. Mpiga piano anaacha kupiga—Mh.]

77 Ninaposhika, usiku wa leo, kijisinia hiki kidogo hapa, ni mkate unaowakilisha mwili wa Bwana wetu, uliofanywa mkate mgumu kwa mikono ya Mkristo. Na sasa unakuja kwetu, kama ishara ya mwili wa Bwana uliovunjwa.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

78 Baba wa Mbinguni, upatanisho huu wa thamani, dhabihu hii uliyotoa kwa ajili yetu, tunaona katika mkate huu, kuteseka na kuraruliwa kwa mwili Wako. Loo, kunaifanya mioyo yetu iugue sana, Bwana, ilie machozi, katika unyenyekevu, wakati tunapofikiri ya kwamba Mungu angefanyika mwili, kusudi apate kujirarua vipandevipande, kufanya upatanisho, kutimiza haki inayotakiwa. Halafu basi, kwa neema, bila ya cho chote hata kidogo, tunaalikwa kuja. Jinsi tunavyokushukuru Wewe, Baba! Utakase mkate huu, sasa, kwa kusudi lake uliokusudiwa na sababu yake. Na mtu ye yote atakayeula, jalia wawe na Uzima wa Milele ukiishi ndani yao. Naomba wasiangamie kamwe, bali waishi milele pamoja na Mungu. Wape afya na nguvu kwa ajili ya safari. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

79 Biblia ilisema, "Vivyo hivyo, akakitwaa kikombe, na baada ya kula, akisema, "Hii ni Damu ya Agano Jipya.' Kila mwinywapo, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo." Ninashika mkononi mwangu tu—tunda la mzabibu. Linawakilisha Damu ya Bwana Yesu.

80 Imesemwa, na wengi, ya kwamba hawawezi kunywa divai, divai ya kawaida, kwa sababu ati ilikuwa ni pombe, ya kwamba ilikuwa ni kinywaji, na ati hawapaswi kunywa divai. Wanakunywa juisi ya zabibu.

81 Sababu ya sisi kunywa divai ni kwa sababu Biblia ilisema, "Divai." Fasiri zote zinasema ni "divai." Sababu nyingine: jinsi divai inavyozidi kukaa, ndivyo inavyozidi kuwa bora zaidi na yenye nguvu zaidi. Juisi ya zabibu huchachuka baada ya masaa machache. Damu ya Yesu Kristo huwa tamu zaidi na bora zaidi jinsi miaka inavyopita. Haichachuki wala haiharibiki.

82 Baba yetu wa Mbinguni, nimeshika kijisinia hiki usiku wa leo, damu ya mizabibu inayowakilisha Damu ya Yesu Kristo. Na sasa, katika jambo hili, mapigo Yake, tuliponywa. Katika Damu Yake tuliokolewa. Na mshairi alisema:

> Bwana, tangu damu Yako
> Kunisafi kale,
> Nimeimba sifa zako,
> Taimba milele.

83 Baba, Mungu, hiyo ndiyo hoja yetu usiku wa leo, pendo la Mungu lililokwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu. Itakase divai hii, Bwana, kwa kazi iliyokusudiwa. Na tunapoinywa, tukumbuke, inawakilisha yale mateso pale Kalvari, wakati ile miiba mikatili, ya dhihaka, ilipochoma uso Wake mpaka ikaitoboa ngozi, na Damu ikatoka. Wakati mjeledi wa adhabu, wenye vikanda tisa vyenye vifundo vya risasi nchani, ulipomcharaza sehemu za mgongoni, mpaka mbavu Zake zikatokeza. Misumari ya kirumi ilipigiliwa kwenye miguu Yake na mikono Yake. Na mkuki ukachoma na kutoboa moyo Wake. Huo ulikuwa ni upendo kwetu sisi tusiostahili.

84 Kwa aibu, tunainama, Bwana, kwamba ilimgharimu Mwana wa Mungu gharama kama hiyo kutukomboa. Halafu jinsi, katika roho zetu, tunainua sifa zetu Kwako, ya kwamba Wewe utupe neema ya kuja, na matumaini. Ulisema, "Mtu awaye yote aulaye mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu yuna Uzima wa Milele, nami nitamfufua tena katika siku ya mwisho." Linawezaje kushindwa wakati lipotoka kwenye midomo kama hiyo! Tutafufuka tena.

85 Kwa hiyo, Baba, usiku wa leo, tunaposimama hapa wenye afya, tujuavyo sisi, na kwa neema Yako, tuna nguvu na wenye afya, na tuna akili timamu, tunakuja kushiriki hii, kukuonyesha Wewe, tunaamini katika mauti, kuzikwa na kufufuka kwa

Bwana wetu. Tunamkubali kama Mwokozi wetu. Tunamwamini kama Mungu na Mfalme wetu.

86 Itakase divai hii, sasa, kwa kusudi lake lililokusudiwa. Na kila mtu anayeinywa, jalia wapokee neema ya Kiungu, Roho Mtakatifu, afya njema na nguvu, kumtumikia Mungu maishani mwao mwote. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

87 [Mpiga piano anaanza kucheza *Damu Imebubujika*. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu Branham na kusanyiko wanakula mkate wa ushirika na divai—Mh.]

Nakutumaini,
Peke Yako;
Nisikie sasa,
Na kunitakasa,
Ni Wako kabisa
Tangu leo!

88 Katika somo la Maandiko, katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu, sura ya 13, tunasoma, kuanzia kifungu cha 2 cha mlango wa 13.

> *. . .baada ya chakula cha jioni; naye Ibilisi sasa amekwisha kumtia Yuda Iskariote, mwana wa Simoni, moyo wa kumsaliti;*
>
> *Yesu, hali akijua. . .Baba amempa vyote mikononi mwake,. . .ya kuwa yeye. . .alitoka kwa Mungu, naye anakwenda kwa Mungu;*
>
> Anaondoka *chakulani,. . .kaweka kando mavazi yake;. . .akatwaa kitambaa, akajifunga kiunoni.*
>
> *Kisha akatia maji katika bakuli,* anaanza *kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga.*
>
> *Hivyo yuaja kwa Simoni Petro. Huyo akamwambia, Bwana, Wewe wanitawadha miguu mimi?*
>
> *Yesu akajibu akamwambia, Nifanyavyo wewe hujui. . .; lakini utalifahamu baadaye.*
>
> *Petro akamwambia, Wewe hutanitawadha miguu kamwe. Yesu akamwambia, Kama nisipokutawadha, huna shirika nami.*
>
> *Simoni Petro akamwambia, Bwana, si miguu yangu tu, hata na. . .hata na mikono yangu na kichwa changu pia.*
>
> *Yesu akamwambia, Yeye aliyekwisha kuoga hana. . . ila ya kutawadha miguu, bali yu safi mwili wote:. . . mmekuwa safi, lakini si nyote.*
>
> *Kwa maana alimjua yeye atakayemsaliti; ndiyo maana alisema, Si nyote mlio safi.*

*Basi alipokwisha kuwatawadha miguu, na kutwaa vazi lake, na kuketi tena, akawaambia, Je! Mmeelewa na hayo niliyowatendea?"*

*Ninyi mwaniita, Mwalimu, na Bwana; nanyi mwanena vema; maana ndivyo nilivyo.*

*Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu wenu, nimewatawadha miguu; imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi.*

*Kwa kuwa nimewapa kielelezo, ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo.*

89 Ninafikiri hicho ni kimojawapo cha vifungu vizuri sana. "Nimewapa kielelezo, kwamba mtende kama nilivyowatendea." Tunapaswa kufanya hivyo sisi kwa sisi, kwa ukumbusho, hivi. Imekuwa ni mazoea ya kanisa, la kundi hili la watu waliokusanyika, tangu tulipoanza. Na kabla maskani hii haijapata kujengwa, wakati tulipokuwa bado tuko katika mikutano ya maombi ya vijijini, tulizoea kutawadhana miguu. Dada zetu huingia katika chumba kimoja huko nyuma. Ndugu zetu wanaingia kwenye chumba cha mkono wa kulia. Nasi tunatawadhana miguu. Enyi wageni, kama mko pamoja nasi, usiku wa leo, tunafurahia tu kuwa nanyi kushiriki katika maagizo haya ya Mungu.

90 Huenda nikaeleza, kama nilivyosema muda mchache uliopita, jambo ambalo Mungu alituachia kufanya. Ubatizo wa maji, agizo moja; ushirika. Na, kumbukeni, hayo ni mawili tu. Mungu hukamilishwa katika utatu. Kutawadhana miguu ndiko kwa tatu. Mnaona? Nasi tunakumbuka jambo hilo, miaka kadha baadaye, hata katika Biblia.

91 Watu wengine wanajaribu kusema si jambo la lazima. Bila shaka, simaanishi kusema ya kwamba miguu ya watu inapaswa kuoshwa. Si hilo. Labda hata yao haikuhitaji kuoshwa pia. Lakini lilikuwa ni tendo la unyenyekevu. Ni te—tendo la—la kufanya, lililo muhimu tu kama ubatizo wa maji. Kwa sababu Yeye amesema hapa, ya kwamba, "Nimewapa mfano, kwamba mnapaswa kufanya hivyo ninyi kwa ninyi kama nilivyowatendea Mimi."

92 Nasi tunaona ya kwamba mjane hangeingizwa miongoni mwa watu isipokuwa alikuwa amewapa wageni nyumba ya kulala na kuosha miguu ya watakatifu, tukijionyesha kwamba sisi ni wanyenyekevu.

93 Hivi kwamba, kama kuna cho chote tunachotaka kuwa, ni kuwa wanyenyekevu, maana hiyo ndiyo siri ya kupata nguvu, ni katika kujinyenyekeza. Nawe daima una furaha, unapotoka kwenye mambo haya, kuyatenda, ni agizo lililobarikiwa la ibada ambayo tunaadhimisha hapa kanisani.

94 Na sasa nataka kutangaza, sasa, ya kwamba usiku wa Jumapili ijayo kutakuwako na ibada hapa. Mara tu nilipoingia, nilipigiwa simu, watu wanakuja kuombewa, kutoka huko mbali Toronto, Canada, watakuwa hapa Jumapili ijayo usiku.

95 Nina kuwekwa wakfu kwa kanisa la Ndugu L. G. Hoover. Liko kwenye ubao wa—ubao wa matangazo. Jumapili ijayo, kwenye saa tano, huko Elizabethtown, Kentucky.

96 Kisha tutarudi hapa kwenye lile lifuatalo, usiku wa Jumapili hii nyingine ijayo. Na kisha tutaenda huko Shreveport, kutoka hapo.

97 Nasi tuna furaha kuwa pamoja nanyi nyote siku nzima. Na nyakati ambazo sisi . . . Wakati, kama mko hapa karibu, mjini, po pote karibu, njoni. Tunataka kukutanika na kukusanyika pamoja. Tunataka kuketi chini ya mafundisho ya ndugu yetu hapa, Ndugu Neville, na—na kushiriki katika mambo yaliyo ya Mungu. Anapoyapata kutoka kwa Mungu, yeye huyatoa. Na—na tunataka kujifunza kutoka kwa Mungu. "Na tunapoona ile siku ikikaribia, hatuna budi kukusanyika pamoja mara nyingi." Hatuna budi kupenda, ndani ya mioyo yetu, kuja kanisani. Kama hatulipendi kanisa, kumpenda Mungu . . . Kukusanyika pamoja, kile tunachoita kanisa, ni kukusanyika kuabudu. Unaona? Kama tunampenda Kristo, tunaabudu tena.

98 Wazia juu ya mtu kusema anampenda mkewe, na kama hakuwa amemwona kwa muda mrefu, apite hapo karibu na kusema, "Vema, nitamwona wakati mwingine"? Unaona? Hampendi. Ama, mke akisema anampenda mumewe, ama wazazi wakisema wanampenda mtoto wao, vema, ina—inaonyesha. Unaona?

99 Nami ninafikiri kujieleza kwetu, kwamba tunapaswa kuwa na shauku sana ya kuabudu, mahali po pote, kumwabudu Bwana, tunapokutanika pamoja kumwabudu Yeye. Kumwabudu nyumbani. Kumwabudu tunapoendesha magari yetu. Po pote tulipo, tumwabudu Bwana, kuomba tu.

100 Biblia ilisema, "Na kila kitu chenye pumzi na kimsifu Bwana." Kisha akasema, "Msifuni Bwana." Hata kama huna pumzi yo yote, hata hivyo msifu Bwana. Unaona? Msifu! "Kila kitu kilicho na pumzi, kimsifu Bwana." Na, halafu, "Msifuni Bwana." Nafikiri, Zaburi 100, Zaburi ya 100.

101 Sasa, Bwana awabariki. Na tunapoimba sasa, tena, ndugu wataingia kwenye chumba *hiki*, na akina dada kwenye chumba *kile*, kwa ajili ya kutawadhana miguu, tunaposimama sasa tupate kufumukana.

102 Nanyi ambao hamna budi kuondoka, mbona, m—mtaruhusiwa kuondoka katika dakika moja. Lakini, basi, tutawaalika kwa furaha kwenye ibada yo yote tuliyo nayo. Njoni, nasi tutajaribu kuwatendea vizuri sana tujuavyo, kuongoza nafsi zenu kwenye mguu wa Yesu Kristo.

Peleka Jina la Yesu,
Ko kote uendako;
Litafurahisha moyo,
Peleka uendako.

Dha-. . .

Sasa geukeni na kupeana mikono, kila mmoja.

. . . .na tamu!
Ni Jina Lake . . .

103 [Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani juu ya kumwambia Ndugu McKinney aombe—Mh.]

. . .Na tamu!
Ni Jina Lake Yesu.

Sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu, tuimbe.

Peleka Jina la Yesu,
Liwe silaha zako;
Utakapojaribiwa,
Lilia Jina . . .

[Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani—Mh.]

Thama-. . .Thamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, na tamu!
Ni Jina . . .

104 [Ndugu Branham anamwambia Ndugu McKinney, "Ninakuomba, uwaruhusu wapumukane, tafadhali."—Mh.]

. . .Lake Yesu.

105 Sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu, kwa unyenyekevu, tunamuuliza Ndugu McKinney hapa kuturuhusu tupumukane kwa maombi. Na mara baadaye, ninyi ambao hamna budi kuondoka, mnaweza kuondoka. Wengine watakusanyika vyumbani. Mungu awabariki.

Ndugu McKinney.

*KUWEKA MHUDUMU* SWA62-1104E
(Ordination)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, 04 Novemba, 1962, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2003 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2003 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org